

## **Maisha Halisi ya Kiroho**

Kuwa Mkristo wa Warumi 12

Sehemu ya 4 – Kiasi katika Kujitathmini Mwenyewe

**Jinsi ya Kujielewa Mwenyewe**

**Kiuhalisia**

Warumi 12:3 - 8

### **Maswali matatu tunayojiuliza sote:**

1. Je, mimi ni nani? (Utambulisho)
2. Je, mimi ni wa wapi? (Usalama/Kujiamini)
3. Je, ninapaswa kufanya nini? (Umuhimu)

## **Kwa nini ni vigumu kujibu maswali haya?**

<sup>8</sup>Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; mume na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone.

<sup>9</sup>Bwana Mungu akamwita yule mwanamume, akamwambia, Uko wapi?

<sup>10</sup>Akasema, "Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha."

<sup>11</sup>Akasema, "Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?

<sup>12</sup>akasema, "Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala."

<sup>13</sup>Bwana Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala.

Mwanzo 3:8-13

## **Vikwazo vitatu vinavyozuia kupata majibu sahihi:**

1. Hofu iliyojikita ndani ya **AIBU**.
2. Kujificha kulikojikita ndani ya **UKOSAJI WA USALAMA/KUTOJAMINI** .
3. Kulaumu kulikojikita ndani ya **KUKANA**.

## **Majibu ya Mungu:**

Warumi 12:3-8

### **1. Je, wewe ni nani?**

Warumi 12:3

*Kwa maana kwa neema niliyopewa namwambia kila mtu aliyeko kwenu: Usinuiie makuu kupita ilivyompasa kunuia; bali uwe na nia ya kiasi, kama Mungu alivyomgawia kila mtu kiasi cha imani.*

Amri: Fikiria **KWA USAHIHI** juu yako mwenyewe

### **2. Je, wewe ni wa wapi?**

Warumi 12:4-5

*<sup>4</sup>Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; <sup>5</sup>Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake.*

Sababu: Una **JUKUMU** la kutekeleza.

### **3. Je, unapaswa kufanya nini?**

Warumi 12:6-8

*<sup>6</sup>Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema tuliyopewa; ikiwa ni unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya imani; <sup>7</sup>ikiwa ni huduma, tuwemo katika huduma yetu; mwenye kufundisha, katika kufundisha kwake; mwenye kuonya, katika kuonya kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; msimamizi, na asimamie kwa bidii; anayerehemu, na arehemu kwa furaha.*

Mazoezi: Gundua na **UTUMIE** karama yako ya kiroho.

## **Usisahau wewe ni nani kiuhalisia!**

1. Mungu alikuumba kwa njia ya kipekee-Una **THAMANA YA MILELE.**

Zaburi 139:13-14

2. Mungu alikuweka katika familia Yake-Una **KUBALIWA BILA MASHARTI.**

Waefeso 3:19-22

3. Mungu alikupa karama ya kutimiza kusudi lake - wewe ni **WA MAANA NA PENG/NAFASI YAKO HAIWEZI KUJAZWA NA MWINGINE.**

Waefeso 2:10

### **Maswali ya Matumizi ya Kibinafsi:**

1. Kwa kipimo cha 1 - 5, Je, unajifikiria kwa usahihi wa kiasi gani?  
Kwa nini? Ikiwa la, kwa nini?

2. Kwa kipimo cha 1 - 5, Je, una uhusiano gani na waumini wenzako?  
Kwa nini? Ikiwa la, kwa nini?

3. Je, karama yako ya kiroho ni ipi? Je, unapenda kufanya nini miongoni mwa watu wa Mungu kuona kwamba kinatumika kuwasaidia na kuwatia moyo wengine?

4. Je, ni "hatua" gani inayofuata unahisi Mungu anataka uchukue ili kukuza kujitathmini kwako kwa kiasi zaidi?

### **Rasilimali kutoka Living on the Edge za Kukusaidia Kutumia Warumi 12:3-8**

*Your Divine Design* – Chip Ingram

*Stop Faking It!*,-(CD- mfululizo wenye sehemu 4)- Chip Ingram

*For Women: Precious in His Sight* – Theresa Ingram